PRESIDENT'S OFFICE

REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

ADVANCED CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION EXAMINATION

MTIHANI WAKABLA YA UTAMILIFU KIDATOCHA SITA

(SHULE YA SEKONDARI IAFAKARA)

KISWAHILI 2

# MUONGOZOWAUSAHIHISHAJI

1. Swali linahitaji mwanafunzi aeleze sifa za fasihi simulizi

(i) Hufungamana na utendaji ii Fanani na hadhira huonana

(iii) Huendana na wakati na mazingira

(iv) Hupokea mabadiliko ya papo kwa papo

(v) Humilikiwa na jamii nzima

(vi) Huwasilishwa kwa njia ya mdomo au masimulizi (@02 = 10 Alama)

2. Swali linamtaka mwanafunzi aeleze sifa za Riwaya pendwa

   (i) Matumizi ya taharuki

   (ii) Mhusika mkuu hukwezwa

   (iii) Dhamira zake zinapendwa sana

   (iv) Mwanamke hutumika kama chombo cha staterehe

   (v) Matumizi ya wahusika walewale

   (vi) Mandhari yake ni ya kipekee (@02 = 10 Alama)

3. Mwanafunzi aeleze maana ya dhana zifuatazo

(i) Mhusika kivuli ni mhusika ambaye hutajwa tu katika kazi ya fasihi bila kutolewa maelezo ya kutosha

(ii) Mahadhi(Tuni) ni sauti mahusussi ya uimbaji wa nyimbo

(iii) Kongozi ni nyimbo zinazoimbwa kwa lengo la kuaga na kukaribisha mwaka

(iv) Taniaba ni tamathali ambapo jina la mtu binafsi hutumiwa kwa watu wengine wenye tabia, mwenendo, hali au kazi sawa na ya mtu huyo.

(v) Taswira ni picha inayojengwa akilini mwa hadhira au mtu.

(@02 = 10 Alama)

4. Mbinu za kifani

(a) Muundo

Muundo wa moja kwa moja.

(b) Mtindo

Mtindo wa masimulizi

Matumizi ya nyimbo

Matumizi ya nafsi zote tatu

Matumizi ya monolojia. (01 Alama)

(c) Wahusika

Maimuna, Mtangazaji, Bwana Maksudi ans Rashidi (01 Alama)

(d) Mandhari

Mandhari ya ukumbini (01 Alama)

(e) Matumizi ya lugha

Mwandishi ametumia lugha fasaha na inayoeleweka

(i) Methali

La kwanza si waungwana na la pili sio mila

(ii) Tamathali za semi

Tashbiha muziki ulianza kugongwa kwa mahdhi ya rumba

(02 Alama)

(iii) Mbinu nyingine za kisanaa (02 Alama)

Takriri

- yale yale
- Tazama tazama

Mdokezo

- Ikakatika shingo kichwa…

Tashtiti

- "tazama mzee yule anakwenda wapi"

Nidaa

- Ana wazimu nini

Mjalizo

- Koti, kelele, mbinja, vicheko, furaha, vigelegele

5. Mwanafunzi anatakiwa kueleza mitindo mbalimbali iliyotumika katika Diwani

CHUNGU TAMU

(i) tindo wa kimapokeo unaofuata urari wa vina na mizani kupitia mashairi ya Fikra za waungwana

* Mfereji maringo
* Chini ya mti mkavu

(ii) Mtindo wa kisasa usiofuata urari wa vina na mizani kupitia mashairi ya

* "chatu na kuku"
* "Chungu tamu"
* "Thomas na Dotto"

(iii) Mtindo wa masimulizi mshairi anamuumba mhusika katika shairi akisimulia hadithi

* "Thomas na Dotto"
* "Chatu na kuku"
* "Manzese mpaka Ostabei"

(iv) Mtindo wa tenzi

* "kademokrasia katoweka"
* "Wabaki taabani"
* "Tutakukumbuka daima"

(v) mtindo wa kidato baadthu ya mistari iliyofupishwa maneno, silabi

* Chungu Tamu
* Manzese mpaka Ostabei
* Wanajua kuvumilia vi Mtindo wamajibizano wasanii kuumba wahusika wa kazi za kifasihi wanaozungumzwa kwa kupokezana
* "Chatu na kuku"
* "Daktari Askari"

KIMBUNGA

(i) Mtindo wa kimapokeo kupitia mashairi ya

* Kiswahili
* Wazazi

* Kibwangai

(ii) Mtindo wa masimulizi mshairi huamua kusimulia hadithi yeye mwenyewe au huwaumba wahusika wanaosimulia. Mashairi ya

* "Kimbwangai"

(iii) Mtindo wa kuhoji mshairi huulia swali ambayo majibu yako wazi au hayakowazi

* "Nimuite jina gani"
* "Mnapata kitu gani"

(iv) Mtindo wa nafsi mshairi hutumia nafsi ya umoja, uwingi au ya kikundi

Mtindo wa nafsi

* Kipaji
* Kurumbizi
* Hili mnatutakiya

| | |
|---|---|
| Utangulizi | (02 Alama) |
| Kiini | (@02 = 16 Alama) |
| Hitimisho | (02 Alama) |

6. Swali linamtaka mwanafunzi aeleze malalamiko ya wasionacho

KIVULI KINAISHI

(i) Malalamiko ya uongozi mbaya
(ii) Maalamiko ya Rushwa
(iii) Malalamiko ya umasikini
(iv) Malalamiko ya Imani za kishirikina za wenye nacho

MORANI

(i) Malalamiko ya usaliti
(ii) Malalamiko ya uujumu uchumi
(iii) Malalamiko ya uongozi mbaya
(iv) Malalamiko ya udhurufu kwa watoto

NGUZO MAMA

(i) Malalamiko ya matabaka
(ii) Malalamiko ya usaliti
(iii) Malalamiko ya rushwa
(iv) Malalamiko ya dhuluma

Mwanaunzi anaweza kutoa hoja nyinginezo zitakazo endana na swali

| | |
|---|---|
| Utangulizi | (02 Alama) |
| Kiini | (@02 = 16 Alama) |
| Hitimisho | (02 Alama) |

7. Swali linataka mbinu za ujenzi wa jamii mpya

- FUNGATE YA UHURU

(i) Kupiga vita matabaka (fungate waja wa mungu, viongozi wa Afrika)
(ii) Kupinga vita uongozi mbaya (fungate ya uhuru ningekuwa na sauti)
(iii) Kupiga vita rushwa (Viongozi wa Afrika)
(iv) Kupiga vita wizi(wizi)
(v) Kupiga vita usaliti (Tumesalitiwa)

- CHUNGU TAMU

(i) Kupiga vita uongozi mbaya (tishio la binadamu, kurumilia)
(ii) Kupiga vita matabaka (wimbo wake hotubani, Thomasi na Dotto)

(iii) Kupiga vita dhuluma (chatu na kuku)
(iv) Kua na mapenzi ya kweli (Daktari askari, Thomasi na Dotto)
(v) Kufanya kazi kwa bidii (Daktari askari, chatu na kuku)

- KIMBUNGA

(i) Kupiga vita uongozi mbaya (Kimbunga)
(ii) Kua na mapenzi ya kweli (Usoimpige mkeo sitaki)
(iii) Rushwa na wizi (Paka)
(iv) Kuwathamini wazazi (wazazi)

8. Mwanafunzi aonyeshe taswira/Jazanda mbalimbali kupitia kazi za waandishi wawili

VUTA N'KUVUTE

(i) Taswira ya Giningi inawakilisha ngoma ya wachawi
(ii) Taswira ya mtoto mbichi inawakilisha msichana ambae ni bikira yaani hajashiriki
(iii) Taswira ya makoo inawakilisha mwanamke
(iv) Taswira ya toto zuri la dunia inawakilisha msichana mzuri sana

USIKU UTAKAPOKWISHA

(i) Taswira ya kunguni, inzi, mende, panya, viroboto inawakilisa mazingira au makazi duni ya watu
(ii) Taswira ya usiku ianwakilisha matatizo au shida walizonazo wananchi
(iii) Taswira ya kamasi inawakilisha maisha magumu waliyonayo wananchi
(iv) Taswira ya giza inawakilisha uwezeano hafifu wa walalahoi/masikini

| | |
|---|---|
| Utangulizi | (02 Alama) |
| Kiini | (@02 = 16 Alama) |
| Hitimisho | (02 Alama) |